# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Anuani ya simu"
Simu: +255 (0) 764784770
Barua pepe:
bigwafdc@moe.go.tz

Chuo cha Maendeleo ya
Wananchi Bigwa,
Mtaa wa Kindibwa.
Jengo Na. 04,
S.L.P 339,
**MOROGORO**.

**Unapojibu tafadhali taja:**

**Kumb. Na. CMW/BG/SG/15/…**

04/11/2025

………………………………….....

YAH: **KUJIUNGA NA CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI BIGWA**

Husika na Kichwa cha barua tajwa hapo juu.

2. Uongozi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa kilichopo Mkoani Morogoro, Manispaa ya Morogoro Mjini, unapenda kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujinga na chuo hiki kwa mwaka wa masomo 2026/2027.

3. Aidha, Chuo kitafunguliwa tarehe **19/01/2026**, mwisho wa kuripoti chuoni ni tarehe **06/02/2026**. Fomu ya kujiunga na chuo imeambatanishwa kwa maelezo zaidi juu ya gharama za mafunzo pamoja na michango.

4. Nakutakia kila kheri katika maandalizi yako ya kuripoti.

Monica Lukeha

**Mkuu wa Chuo**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**FOMU YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA MUDA MREFU CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI BIGWA KWA MWAKA WA MASOMO 2026**

## A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI

**Jina Kamili La Mwanafunzi………………………………………………………………………………………**

**Jinsia (Weka Alama ✓ ) ☐ Me ☐ Ke**

**Tarehe Ya Kuzaliwa (DD/MM/YYYY) ……………………………………………………………………………**

**Anuani Yako ………………………………………………………………………………………………………………**

**Unakotoka: Wilaya…………………………………………Mkoa ……………………………………………**

**Kiwango cha Elimu...........................................Namba ya Mtihani wa kidato cha Nne..............................**

**Jina la mzazi.....................................................Namba Ya Simu Ya Mzazi………….............................**

**Jina la Mlezi.......................................................Namba ya Simu...................................................................**

## B: FANI ZA UFUNDI STADI- NGAZI YA I &II ( chagua fani moja tu)

i. Umeme wa Majumbani ( )
ii. Ufundi Magari, ( )
iii. Useremala, ( )
iv. TEHAMA /ICT ( )
v. Mapishi na Lishe ( )
vi. Mifugo ( )
vii. Kilimo ( )
viii. Uashi, ( )
ix. Ushonaji ( )
x. Uungaji Vyuma & Uchomeleaji ( )

Aidha, pamoja na fani hizo zilizoainishwa hapo juu, washiriki watajifunza masomo mtambuka (Ujasiriamali na stadi za maisha) na masomo ya uelewa kulingana na mahitaji ya fani husika. Masomo hayo ni pamoja na; **Lugha ya Lugha ya Kiingereza,Hisabati,Uchoraji Sanifu,Sayansi ya uhandisi,matumizi ya kawaida ya Kompyuta,Sayansi ya Wanyama,Sayansi ya Udongo, Lugha ya Lugha ya Kifaransa, na Utalii.**

**N.B: Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kiingereza.**

**C: ADA NA MICHANGO YA CHUO**

| NA | MAHITAJI | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Ada | 100,000/= |
| 2 | Vifaa vya Mafunzo | 250,000/= |
| 3 | Ukarabati kinga | 40,000/= |
| 4 | Huduma ya kwanza | 10,000/= |
| **Jumla Kuu** | | **400,000/=** |

**N.B** Ada **Tshs. 100,000/=** ilipwe kwenye mfumo wa Serikali na mwanafunzi atalazimika kupata **Control Number** toka chuoni ili afanye malipo pindi anaporipoti.

Michango ya Chuo **Tsh**. **300,000/=** ilipwe kwenye akaunti ya chuo **22101100068** Benki ya **NMB**

Jina la Akaunti: **CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI BIGWA**.

**Muhula wa kwanza mwanafunzi atapaswa kulipa Tsh 300,000/= (Ada 100,000/= na Michango ya Chuo 200,000/=** na **Muhula wa pili Tsh 100,000/=** Aidha, Mwanachuo hatapokelewa asipofikisha kiwango cha **Tsh. 300,000/= kwa muhula wa kwanza**.

**TAREHE YA KUFUNGUA CHUO NI 19/01/2026 kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri.**

**MWISHO WA KURIPOTI CHUONI NI TAREHE 06/02/2026 Saa 9:30 Alasiri.**

GHARAMA YA FOMU HII NI **TSH 10,000/=** ILIPWE KWENYE **AKAUNTI NAMBA 22101100068 BENKI YA NMB** Jina la Akaunti: **CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI BIGWA** MWANAFUNZI ANAPORIPOTI CHUONI ATAPASWA KUWASILISHA BANK SLIP YA MALIPO YA FOMU HII

**Kwa mawasiliano zaidi :**

**Website:https://www.bigwafdc.ac.tz** **Mkuu wa Chuo +255764 784 770**

**E-mail:bigwafdc@moe.go.tz** **Mratibu mafunzo +255713 423 475**

MONICA LUKEHA

**MKUU WA CHUO**

**NB:**

- **FEDHA IKISHALIPWA HAIRUDISHWI**
- **MWANACHUO ATAPATA HUDUMA YA CHAKULA CHUONI BURE.**
- **KAMA UMEKUBALI KUJIUNGA NA CHUO CHA BIGWA FDC TUMA UJUMBE WA MESEJI KWA NAMBA 0741-234-234**

**D: MAHITAJI MENGINE YA MWANACHUO:**

1. Sare ya Chuo:-
   a) Shati jeupe mikono mirefu.
   b) Suruali (Rangi nyeusi) zinashonwa chuoni na si sehemu nyingine kwa gharama Tsh 25,000/=
      - Urefu wa suruali iguse kiatu
      - Upana wa Suruali ni 17-18
      - Suruali iwe na rinda mbili (2) mbele)
   c) Sweta la Rangi Nyeusi
   d) Overall ambayo ni sare ya Chuo rangi ya dark blue (Kwa fani ya ufundi magari, na Uashi)
   e) Overcoart (kwa fani ya ushonaji, Kilimo, Umeme,Tehama,Useremala na Uungaji vyuma) kwa fani ya mifugo aje na overcoat jeupe na suruali nyeupe.
   f) T –shirt ya chuo inapatikana chuoni kwa gharama ya Tsh. 20,000/=
   g) Apron,kofia na raba nyeusi (kwa fani ya Mapishi na lishe)
   h) Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi na soksi nyeupe.
   i) Tracksuit ya Dark Blue na Raba Nyeupe kwaajili ya michezo.
2. Mwanachuo mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea aje na kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA (Lazima) kwaajili ya kutengenezea Bima ya Afya.
3. Kwa Wanachuo ambao hawana kadi za Bima ya Afya NHIF waje na pesa **Tsh 50,400/=** kwa ajili ya kulipia bima ya afya (NIHF) ili kupata matibabu Katika hospitali zote nchini zilizosajiliwa na mfuko huo,au njoo na Bima yako ya NHIF kama unayo.(**Zingatia asiye na Bima ya NHIF au Fedha Hatapokelewa)**
4. Madaftari yasiyopungua 10, kalamu za wino na kalamu ya risasi pamoja na mkebe.
5. Kwa Mwanachuo wa Bweni aje na vyombo vya kutumia :- Sahani ya bati, Bakuli, Kikombe, Kijiko na Ndoo, pamoja na **neti ya mbu (nyeupe**) na **mashuka mawili (2) rangi ya blue**
6. Godoro lenye **size 2½ x 6** kwa wanachuo wa bweni**.**
7. Vitu vyakuja navyo kulingana na fani ni ;
   **i.** UMEME (EL) - Screw driver 1 ya star, screw driver 1 flat, test 1, combination playa 1 , nyundondogo 1 namultimita moja kubwa.
   **ii.** MAGARI (MVM)- set moja ya spana za kufungulia
   **iii.** KILIMO (HCFCP)- Tape meter 20
   **iv.** MIFUGO (AH)- Outomatic sindano 1
   **v.** USHONAJI (DSCT)- sindano za chelehani box 1, mkasi 1, tape measure 1
   **vi.** UASHI (MBL) - mwiko 1, konobao 1, pima majina tape measure meter 5
   j) TEHAMA (ICT) – Flash Disk at least 8GB, Precision Screwdriver Set, Electric gloves & Reflector jacket.
8. Mwanachuo wa Bweni aje na pesa kwa ajili ya matumizi yake binafsi na nauli za kurudi Nyumbani wakati wa likizo.
9. Vifaa vya usafi : Soft bloom 1, hard bloom 1, Kwanja 1, Reki 1, Squizer 1, Panga 1, Jembe 1 lenye mpini pamoja, Fagio ya chelewa 1 na Sabuni ya maji (original) moja aina ya DEXI au TARMOL
10. Safety boot nyeusi (lazima) kwaajili ya mazoezi ya vitendo kwa fani zote isipokuwa fani ya Ushonaji.
11. Rimu 2 A4 Double A (Rimu moja italetwa wakati mwanafunzi anaripoti na rimu ya pili italetwa muhula wa pili Julai),
12. Waliohitimu form 4 waje na nakala (copy) ya cheti au namba ya mtihani wa fomu four. (lazima)
13. Mwanachuo aje na PREMU NAMBA, kwa waliohitimu Elimu ya Darasa la Saba.

# HATI YA SHERIA ZA CHUO CHA MAENDELEO YA WANANCHI BIGWA

Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa kinaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu. Aidha, kinazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti Chuoni.

## 1. TAALUMA

a. Mwanachuo anapaswa kuhudhuria Chuoni kila siku za masomo na atawajibika kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa, pamoja na kufanya mtihani masomo yote ya ndani na nje **kutokufanya mitihani au kutokuhudhuria darasani kwa zaidi ya vipindi vitatu bila sababu zamsingi ni kosa mwanachuo atasimamishwa masomo au kufukuzwa Chuo**.

b. Mwanafunzi anapaswa **kufaulu mitihani kwa kiwango cha daraja "C" lenye ufaulu wa asilimia 60%** kufeli mtihani ni kosa mwanafunzi atapata adhabu zitakazopendekezwa kwa wakati huo, Aidha, ataandika barua ya kuahidi kubadilika na kufanya vizuri kwenye mtihani**.**

c. **Udanganyifu** wa aina yoyote katika mitihani haurusiwi mwanachuo akibainika **atafukuzwa Chuo**.

d. Kutakuwa na Mtihani wa Taifa ambao utafanyika mwisho wa mwaka, gharama za mtihani zitatolewa pindi mtihani unapokaribia.

e. Ni marufuku kupiga kelele, kusumbua darasani, kutoka nje ya darasa bila ruhusa ya mwalimu,adhabu kali zitatolewa ikiwemo kuchimba shimo/kulima matuta mawili/kufyeka.

f. Mwanachuo **harusiwi kuingia na simu darasani au kutumia simu muda wa masomo pia hairusiwi kuchaji simu bwenini ikibainika atachukuliwa adhabu kali** ikiwemo kunyang'anywa simu.

g. Mwanachuo wa bweni haruhusiwi kutoka nje ya eneo la Chuo bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwalimu wa zamu au mlezi wa darasa,Mwanachuo anapaswa ahudhurie paredi ya Chuo saa 11:00 jioni siku za "weekends"hatua za kinidhamu zitachukuliwa ikiwemo **kusimamishwa masomo au kufukuzwa Chuo na atapoteza sifa ya kukaa bweni** endapo itabainika hukufuata utaratibu huu**.** Aidha kibali cha kutoka nje ya chuo **hakitatolewa baada ya saa kumi na mbili jioni.**

h. Mwanachuo anapaswa kutii kengele ya Chuo kulingana na utaratibu au ratiba ya Chuo na dharura zinazojitokeza kupuuzia wito ni utovu wa nidhamu adhabu na atapewa adhabu kama vile Kung'oa kisiki/visiki, Kufukia mashimo hatarishi, Kusafisha shamba/kulima/ kufyeka

i. Mwanachuo anapaswa kutii bendera ya Taifa na wimbo wa taifa.

j. Mwanachuo anapaswa kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za chuo kama vile usafi wa mazingira n.k hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kama hatazingatia utaratibu.

k. Kutakuwa na vipindi vya kujisomea kuanzia saa 2:00 usiku hadi 4:00 usiku kila mwanachuo anatakiwa kuwepo darasani.Mahudhurio yatachukuliwa na adhabu kali zitatolewa kwa wasiohudhuria vipindi vya kujisomea ikiwemo kuchimba shimo, kufyeka, kuandaa tuta la bustani.

l. Kutakuwa na likizo 4 kwa mwaka kufuatana na kalenda ya masomo,hivyo mwanachuo anatakiwa kutunza fedha ya nauli ya kurudi nyumbani pindi Chuo kikifungwa, mwanachuo haruhusiwi kubaki chuoni wakati wa likizo bila kibali cha chuo.

m. Mwanachuo harusiwi kulala bwenini saa za masomo bila kibali cha Muuguzi wa Chuo kwa kisingizio cha kuumwa taarifa za ugonjwa zitatolewa kwa Muuguzi wa chuo au mwalimu wa zamu ndipo mwanachuo anaruhusiwa kwenda kupumzika. Mwanafunzi atakayelala bwenini muda wa masomo bila kibali cha Muuguzi/mwalimu wa zamu atahesabika kama mtoro wa vipindi na hivyo atapewa adhabu ikiwemo , kubeba kifusi, kuchimba shimo au kupoteza sifa ya kukaa bweni.

## 2. SARE

a. Mwanachuo anapaswa kuvaa sare ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa pamoja na kitambulisho wakati wote akiwa nje na ndani ya Chuo.Pia mwanachuo anatakiwa kuvaa sweta jeusi kama sare ya Chuo kipindi cha baridi muda wote wa masomo. Aidha nje ya muda wa masomo anatakiwa avae nguo za heshima (mavazi yasio ya heshima hayaruhusiwi mfano suruari za kubana,sketi fupi na nguo zinazoonesha maumbile ya mwili n.k)

b. Wakati wa michezo, Mwanachuo anapaswa kuvaa jezi za michezo (Tracksuit)

c. Siku ya Alhamisi mwanafunzi anapaswa kuvaa T-shirt na suruali nyeusi, Mwanachuo anapaswa kuchomekea shati lote.

d. Mwanachuo haruhusiwi kufuga **ndevu**,wala **kunyoa mitindo,kuweka nywele dawa,kufuga kucha au kupaka rangi ,**hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa ikiwemo kupewa adhabu kali pamoja na kunyolewa .

e. Mwanachuo haruhusiwi kuvaa chochote masikioni, shingoni, puani na mkononi isipokuwa saa ya mkononi tu, ikibainika atanyang'anywa alichovaa ikiwa ni pamoja na kupewa adhabu.

f. Mwanachuo anatakiwa kuwa msafi wakati wote, haruhusiwi kutumia **manukato** na **vipodozi** vinavyotoa harufu kali kiasi cha kuwasumbua wengine wakati wote wa masomo.

g. Wasichana wenye nywele ndefu zikatwe urefu usizidi 0.5 cm, au zisukwe kwa mstari ( twende kilioni nywele tano mpaka nane)

h. Wavulana wakate nywele urefu usiozidi 0.5 cm na ndevu zinyolewe wakati wote.

## 3. NIDHAMU

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanachuo wengine, viongozi wa serikali ya wanachuo na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b. Mwanachuo anatakiwa kuiheshimu bendera ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Nembo ya Taifa, na Wimbo wa Taifa.

c. Ulevi wa aina yoyote mfano **pombe, sigara, madawa ya kulevya** havirusiwi ikibainika mwanachuo **atafukuzwa Chuo maramoja**

d. Uhusiano wa **kimapenzi** chuoni kati ya mwanachuo na mwanachuo au mtumishi na Mwanachuo hauruhusiwi kabisa ikibainika mwanachuo atafukuzwa chuo.Aidha mtumishi atachukuliwa hatua kali za kinidhamu kwa mujibu wa kanuni za maadili kwa watumishi wa Umma.

e. Hairuhusiwi kubeba mimba uwapo chuoni. Ikitokea muhusika atasimamishwa mafunzo kwa muda na ataruhusiwa kurudi chuoni mara baada ya kujifungua ikiwa ni pamoja na kumuacha mtoto nyumbani.

f. Lugha ya matusi,ugomvi wa aina yoyote, **kupigana, kufanya fujo** haviruhusiwi ikibainika sheria kali zitachukuliwa ikiwemo kufukuzwa chuo.

g. Vitendo vya wizi, uhalifu haviruhusiwi kabisa ikibainika atafukuzwa Chuo maramoja na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola.

h. Hairuhusiwi **kugoma au kuchochea migomo** ikibainika mhusika **atafukuzwa Chuo**, Tatizo lolote litatuliwe kwa vikao halali.

i. Hairuhusiwi **kuharibu kwa makusudi mali ya Chuo au jamii inayozunguka chuo muhusika atasimamishwa chuo ikiwemo kulipa gharama za uharibifu.**

j. Mgeni atakayekutembelea sharti apate kibali kutoka Uongozi wa Chuo. Ni marufuku kumtembeza mgeni yoyote katika maeneo ya Chuo bila kibali cha Uongozi wa Chuo**.**

k. Lugha inayotumika kuwasiliana ni Kiswahili na kiingereza tu.

**4. MAZINGIRA**

a. Kila mwanachuo katika miaka yote hapa chuoni atatakiwa kupanda na kukuza angalau mti mmoja wa kudumu ambao atatakiwa kuukabidhi wakati atakapomaliza chuo

b. Kila Mwanachuo atagawiwa eneo lake maalum (Special Area) ambalo atalitunza kwa usafi mpaka atakapomaliza chuo.

c. Kila mwanachuo atakuwa na zamu ya kufanya usafi katika Bwalo la chakula, Darasani, Vyooni na bwenini kutokushiriki usafi ni kosa adhabu itatolewa kwa watakao kaidi.

d. Kila siku ya Ijumaa kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi 3:00 asubuhi itakuwa ni muda wa usafi maalumu, Aidha, kila siku za wiki utafanyika usafi wa mazingira yote kwa ujumla.

**5. MAENEO YASIYORUHUSIWA KUFIKA MWANACHUO**:

**Mwanachuo haruhusiwi kufika/kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalum**:- **ikibainika mwanafunzi atafukuzwa chuo/ kupewa adhabu kali**

Ofisi za chuo bila ruhusa. Bohari za chuo, Jikoni bila ruhusa, Baa, Klabu au sehemu yoyote panapouzwa vileo, Nyumba za kulala wageni, Nyumba za watumishi bila sababu maalumu, Bwalo endapo kuna shughuli za kijamii na mikutano, bweni la wasichana kwa mwanafunzi wa kiume, na bweni la wavulana kwa mwanafunzi wa kike.

**Siku ya kutoka nje ya Chuo ni siku ya jumamosi kuanzia saa 5:00 asubuhi na jumapili kuanzia saa 3:00 asubuhi kwa ruhusa hadi saa11:00 jioni**.

**N: B: Bandika picha kwenye viboma tajwa hapa chini**

| **Picha ya Mwanafunzi** *(4 x 4.5 cm)* | **Picha ya Mzazi/Mlezi** *(4 x 4.5 cm)* |
|---|---|

Mimi(Mwanafunzi)………………………………………………nathibitisha kuwa taarifa nilizojaza kwenye fomu hii ni za kweli. Ahadi yangu, nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa ya kujiunga na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa pia nina ahidi kufuata sheria na taratibu zote za chuo kama zilivyotolewa kwenye fomu hii na zitakazotolewa na Uongozi wa Chuo nikiuka sheria za chuo ziniwajibishe.

……………………… …………………

Sahihi ya mwanafunzi Tarehe

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi)………………………………………………… ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi………………………………………….nimesoma taratibu na sheria za Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Bigwa. Naahidi kwamba nitamuhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za chuo kama zilivyoelezwa. Aidha, naahidi kushirikiana na Uongozi wa Chuo katika malezi bora ya mwanangu ili baadae awe raia mwema wa Taifa letu.

……………………… …………………

Sahihi ya Mzazi/Mlezi Tarehe

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**BIGWA FOLK DEVELOPMENT COLLEGE**

## STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION FORM

To the Medical Officer ………………………………………………................................................

Mr./Mrs./Miss ………………………………………………………………………………………...

**PERSONAL HISTORY**

First Name ……………….………………………. Other names……………………………………………

Adm. No.…………………………. Course/ ……………………………………………………………...

Age…………Gender……………. Marital Status….………………........................................................

Please examine the above named as to his/her fitness for undergoing the studies.
Date ……..…… 2026

a) Tuberculosis………………………………………………………………….................................

b) Other respiratory diseases…………………………………………………......................................

c) Cardiac Disease ……………………………………………………………....................................

d) Gastro – Intestinal disease…………………………………………………......................................

e) Serious Injuries and allergies……………………………………………….....................................
f) Pregnancy …………………………………………………….............................................................
g) Any Physical challenges of the prospective student plus the Doctor's recommendations

…………………………………………………………………………….......................................

Name ………………………………………………….……….........................................................

Signature………………………………………………….................................................................

Title …………………………………………….. Qualifications
(Official Stamp)